JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA UCHUKUZI

MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI

IMETHIBITISHWA ISO 9001

*“{}*

## HOTUBA YA MKURUGENZI MKUU - LATRA

# HAFLA YA UFUNGUZI WA MAADHIMISHO YA KWANZA YA WIKI YA USAFIRI ENDELEVU ARDHINI 2025, KATIKA KITUO CHA MIKUTANO CHA KIMATAIFA CHA JULIUS NYERERE (JNICC) DAR ES SALAAM TAREHE 26 NOVEMBA, 2025

- **Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Mchemba (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Mgeni Rasmi,**
- **Mhe. Prof. Makame Mbarawa (Mb), Waziri wa Uchukuzi na Mawaziri Mliopo,**
- **Mhe. David Kihenzile (Mb), Naibu Waziri Uchukuzi na Manaibu Waziri Mliopo**
- **Mhe. Albert Chalamila, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam**
- **Prof. Godius W. Kahyarara, Katibu Mkuu, WU na Makatibu Wakuu Mliopo**
- **Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama Mliopo,**
- **Kamati ya Usalama ya Mkoa wa Dar es Salaam,**
- **Bw. Raymond Shoniwa, Mtendaji Mkuu wa Sekretariat ya Umoja wa Reli Kusini mwa Afrika (SARA) na Wadau Wote kutoka Nje ya Tanzania**
- **Viongozi wa Wizara, Wakuu wa Taasisi za Umma na Sekta Binafsi,**
- **Kamati ya Maandalizi ya Maadhimisho haya,**
- **Viongozi na wajumbe wa vyama vya wasafirishaji mliopo,**
- **Watoa Huduma za Usafiri Ardhini,**
- **Watumiaji Huduma za Usafiri Ardhini na Wadau wa Sekta ya Uchukuzi,**
- **Wanahabari,**
- **Wageni waalikwa, Mabibi na Mabwana**
- **Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!**

## 1. SHUKRANI

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Kwa niaba ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kutupa uhai, afya njema, na fursa ya kukutana mahali hapa ili kuadhimisha **Siku ya Usafiri Endelevu Duniani 2025**, na kwa mara ya kwanza kufanya maadhimisho ya **Wiki ya Usafiri Endelevu Ardhini 2025** hapa Nchini.

Pili, tunatoa shukrani maalum kwa Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na Uongozi Mzima wa Serikali ya Awamu ya Sita, kwa Usikivu, na Uongozi Mahiri ulioweka mazingira rafiki sana yaliyojengwa kupitia falsafa ya 4R (**Reconciliation, Resilience, Reforms, & Rebuilding**) katika usimamizi wa sekta ya uchukuzi Nchini ambayo yalikuza shughuli za kiuchumi na kijamii. Wasafirishaji wanamshukuru sana Mhe. Rais kwa kuboresha mazingira ya biashara zao pamoja na kutoa ruhusa ya mabasi kusafiri usiku na mchana 24/7 baada ya zuio la miaka 20 hivyo, kuchochea shughuli za kiuchumi na kijamii.

Tatu, tunakushukuru sana wewe binafsi kwa kukukubali mwaliko wa Waziri wa Uchukuzi, kuwa Mgeni Rasmi kwenye Maadhimisho haya. Tunatambua majukumu yako makubwa, hasa kipindi hiki cha baada tu ya Uchaguzi Mkuu 2025, lakini bado umeweza kutupa thamani na kuwa nasi leo. Hii inadhihirisha mapenzi makubwa ya Serikali ya Awamu ya Sita, inayoongozwa na Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa Watoa Huduma za Usafiri Ardhini.

Mwisho, sio kwa umuhimu, tunawashukuru sana Jeshi la Polisi, Watoa Huduma za Usafiri Nchini (Wamiliki wa Magari, Madereva, Wahudumu – Kondakta na Utingo, Vyuo vya Mafunzo ya Usafiri na Usafirishaji, Watoa Huduma wa Tiketi Mtandao, Watoa Huduma wa Vifaa vya Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTD), Wauza Magari ya Abiria na Mizigo, Vyama vya Wasafirishaji), Watumiaji wa Huduma za Usafiri Ardhini na Baraza lao (LATRA CCC), kwa ushirikiano wao katika kutekeleza majukumu yetu, na pia kwa wote waliokuja kushiriki kwenye maadhimisho haya. Asanteni Sana!

## 2. UMOJA WA MATAIFA KUANZISHA SIKU YA USAFIRI ENDELEVU DUNIANI

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Tarehe 16 Mei 2023, Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa lilipitisha Azimio Na. 77/286 na kuteua tarehe 26 Novemba ya kila Mwaka kuwa **Siku ya Usafiri Endelevu Duniani (**World Sustainable Transport Day). Uamuzi huu wa kihistoria unawakilisha hatua nyingine muhimu katika kukuza ushirikiano wa usafiri endelevu na kuendeleza ahadi ya kimataifa ikijumuisha Malengo ya Maendeleo Endelevu (Sustainable Development Goals – SDGs 2030), na Makubaliano ya Paris kuhusu Mabadiliko ya Hali ya Hewa (Paris Agreement on Climate Change) ya Mwaka 2015, ambazo zinahusu kuboresha usalama wa mazingira pamoja na usafiri duniani. Hivyo, **Siku ya Usafiri Endelevu Duniani** ilianza kusherehekewa kwa mara ya kwanza tarehe **26 Novemba 2023**.

Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa lilizikaribisha Nchi zote duniani, Taasisi za Umoja wa Mataifa, Taasisi za Kikanda na Kimataifa, Jumuiya za Kiraia, ikijumuisha Taasisi zisizo za Kiserikali (NGOs), na wadau wengine wote wa usafiri na usafirishaji, kuiadhimisha siku hii kwa **kutoa elimu na kuandaa shughuli zitakazokuza elimu juu ya masuala ya usafiri na usafirishaji**, hususan aina za **usafiri bora na salama**, kuhamasisha **usafiri unaotunza mazingira**, kujenga **miundombinu ya usafiri inayozingatia watu wenye mahitaji maalum**, na masuala mengine ya **usafiri bora, salama na endelevu**.

Ni kwa mantiki hii, Serikali kupitia Wizara ya Uchukuzi na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), iliamua kuandaa maadhimisho ya Kwanza ya **Wiki ya Usafiri Endelevu Ardhini 2025, tarehe 24-29 Novemba 2025,** sambamba na **Siku ya Usafiri Endelevu Duniani** ambayo ni leo, tarehe **26 Novemba 2025**.

## 3. MAADHIMISHO WIKI YA USAFIRI ENDELEVU ARDHINI-TANZANIA

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Tunafahamu kwamba **Siku ya Kimataifa ya Usafiri wa Majini Duniani** huadhimishwa kila mwaka tarehe **26 Septemba** ambapo hapa Nchini, **Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC)** husimamia maadhimisho hayo chini ya miongozo ya **Shirika la Kimataifa la Usafiri Baharini (IMO)**. Aidha, **Siku ya Kimataifa ya Usafiri wa Anga**

**Duniani** huadhimishwa kila mwaka tarehe **07 Disemba** na hapa Nchini, **Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA)** husimamia maadhimisho hayo chini ya miongozo ya **Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga Duniani (ICAO).**

Hivyo, Serikali ya Awamu ya Sita, inayoongozwa na Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuzingatia misingi ya utawala bora na inayotambua na kuthamini maazimio ya Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa, imeamua kuanzia mwaka 2025 madhimisho haya yafanywe kupitia Wizara ya Uchukuzi na LATRA, kwa jina la **Wiki ya Usafiri Endelevu Ardhini 2025** sambamba na **Siku ya Usafiri Endelevu Duniani 2025**. Kauli Mbiu ya maadhimisho haya ni **Nishati Safi na Ubunifu katika Usafirishaji *(Green Transport and Innovation)*.** Kauli Mbiu hii inasisitiza jukumu muhimu la mifumo ya usafiri shirikishi, yenye ustahimilivu na iliyo rafiki kwa mazingira katika kufikia **Malengo ya Maendeleo Endelevu,** na **Mkakati wa Taifa wa Nishati Safi.**

Kwa kuzingatia ukweli kwamba ufanisi wa huduma za usafiri wa majini na usafiri wa anga vinategemeana na ufanisi wa usafiri ardhini, **TCAA** na **TASAC** ni washiriki katika maadhimisho haya. Aidha, LATRA tumeshirikiana na pacha wetu **Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani ya Zanzibar (ZARTSA).** Taasisi zetu hizi, LATRA, TASAC, TCAA na ZARTSA, zimeshirikiana pia katika maandalizi ya maadhimisho haya, na zote zinashiriki maonesho yanayoendelea Mnazi Mmoja.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**

Maandalizi ya maadhimisho ya **Wiki ya Usafiri Endelevu Ardhini 2025** yamefanywa na Kamati ya Pamoja kati ya Serikali na Sekta Binafsi ikijumuisha Watoa Huduma, Watumia Huduma, na Wadau wa Usafiri na Usafirishaji, chini ya Prof. Godius Kahyarara, Katibu Mkuu, Wizara ya Uchukuzi.

Maadhimisho haya yanajumuisha Mkutano utakaokuwa na **makongamano, midahalo ya kisera, na maonesho ya kazi mbali mbali za wadau** ambapo imewaleta pamoja Waoneshaji (Exhibitors) 63 katika viwanja vya Mnazi Mmoja na washiriki zaidi ya 1,000

kutoka Tanzania Bara na Visiwani, na ukanda mzima wa Afrika Mashariki (EAC) na Jumuia ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) kwenye Kongamano JNICC. Mada zitakazojadiliwa zimejikita kwenye Kauli Mbiu ya Maadhimisho haya. Aidha, washiriki zaidi ya 6,000 wanatarajiwa kuhudhuria maonesho yanayoendelea katika viwanja vya Mnazi Mmoja, Dar es Salaam. Vilevile, siku ya tarehe 28 Novemba 2025, kutakuwa na utalii mfupi kwa washiriki kusafiri kwa SGR (EMU-Mchongoko), kutoka Dar es Salaam (KM 0) kwenda Kituo cha Kwala na Kurudi Dar es Salaam (KM 0).

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**

Maadhimisho haya yamewezekana kwa kuwezeshwa na Wadhamini zaidi ya 30 waliojitolea muda wao na rasilimali fedha. Naomba niwatambue mbele yako na kuwashukuru sana wadhamini wetu wote, na shukrani maalum kwa wadhamini wa makundi yafuatayo:

A. Wadhamini Wakuu – Platinum Sponsors (2) - Kupewa Tuzo
   1) Shirika la Reli Tanzania (TRC)
   2) Kampuni ya DP World Dar es Salaam Limited

B. Wadhamini Daraja la Dhahabu – Gold Sponsors (6) – Kupewa Tuzo
   1) Central Corridor Transit Transport Facilitation Agency (CCTTFA)
   2) Kuenhe Foundation
   3) Tanzania Petroleum Development Authority (TPDC)
   4) Tanzania Shipping Agencies Corporation (TASAC)
   5) YUTONG
   6) Tanzania Electric Mobility Association
   7) BusBora Company Limited

C. Wadhamini Daraja la Fedha - Silver Sponsors (7) - Kupewa Vyeti

1) Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani Zanzibar (ZARTSA)
2) VIA Service
3) OTAPP Agency Company Limited
4) Calabash
5) Hashtech
6) Traxtion Sheltam (Pty)

D. Wadhamini Daraja la Shaba - Bronze Sponsors (4) - Kupewa Vyeti

1) NBC Bank Limited
2) Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Nchini (TIRA),
3) Benki Kuu ya Tanzania
4) Shirika la Bima la Taifa (NIC)

E. Wadhamini Wengine - Kupewa Vyeti

Taasisi za Umma (TPA, TCAA, WCF), Wamiliki wa Mabasi (Shabiby Line, AN Classic, Mtoto Gema, na Tilisho), Web Corporation, Sekretariat ya *Maritime Orgnization of Eastern, Southern, and Northen Africa* (MOESNA)-Mombasa, BRAVO Logistics, na wengine wote kama walivyoorodheshwa kwenye mabango yetu.

## 4. TUZO KWA WATOA HUDUMA NA WADAU WA USAFIRI ARDHINI

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**

Maadhimisho ya Wiki ya Usafiri Endelevu wa Ardhini yanaambatana na utoaji wa tuzo mbalimbali kwa Watoa Huduma na Wadau wa Usafiri Ardhini kutambua na kuthamini michango yao katika Sekta ya Uchukuzi. Wizara ya Uchukuzi kupitia LATRA, ilianza kutoa Tuzo za Wasafirishaji Bora na Salama mwaka 2024 ambazo zilitolewa kwa washindi na Mhe. Dkt Philip Isdori Mpango, jijini Dodoma, katika maadhimisho ya Wiki ya Usalama Barabarani. Hivyo, leo tutakuomba utoe TUZO kwa Watoa Huduma Bora na Salama, pamoja na makundi mengine kwa mwaka 2025. Tuzo hizi zinatolewa kwa kuzingatia jukumu la LATRA kisheria la kukuza ushindani wenye ufanisi kwa kipindi cha kuanzia Julai 2024 hadi Juni 2025.

Vigezo vilivyotumika kuwapata washindi kwa mujibu wa Sheria na kanuni ni pamoja na:

a) Usimamizi wa vyombo vya usafiri pamoja wafanyakazi;
b) Ubunifu na matumizi ya teknolojia;
c) Usalama na huduma bora kwa wateja;
d) Matumizi ya madereva waliothibitishwa na wahudumu waliosajiliwa na LATRA;
e) Utunzaji wa mazingira;
f) ulipaji wa tozo za LATRA kwa wakati sahihi;na
g) uzingatiaji wa Sheria na Kanuni za Usafirishaji, Bima na Usalama Barabarani.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**

Zoezi lilikuwa la awamu mbili, ambapo awamu ya kwanza washindani walichujwa kwa kuzingatia vigezo vilivyotajwa na awamu ya pili ilihusisha kura zilizopigwa na watumia huduma. **Aidha, tutaomba utoe tuzo maalum kwa wadhamini wa maadhimisho haya kwa udhamini uliotolewa.**

**Tuzo zimeandaliwa kwa makundi nane (8) yafuatayo:**

| **Na.** | **Kundi la Kupewa Tuzo** |
|---|---|
| 1. | Wasafirishaji kwa magari ya mizigo ndani ya nchi na nje ya nchi |
| 2. | Wasafirishaji kwa mabasi masafa marefu (Mkoa na mkoa na nchi jirani) |
| 3. | Madereva wa Mabasi ya masafa marefu (Mkoa na mkoa na nchi jirani) |
| 4. | Wahudumu wa Mabasi ya masafa marefu (Mkoa na mkoa na nchi jirani) |
| 5. | Watoa huduma za mifumo ya Tiketi Mtandao (e-Tickets Vendors) |
| 6. | Watoa huduma ya Mifumo ya Ufuatiliaji Mwenendo wa Magari (VTS) |
| 7. | Watoa huduma ya mifumo ya Teksi mtandao (Ride Hailing Platforms) |
| 8. | Wadhamini wa Maadhimisho<br>• Wadhamini Wakuu<br>• Wadhamini Daraja la Dhahabu – Gold Sponsors |
| | Tuzo za Wanahabari na Vyombo vya Habari *(Matokeo kupelekwa Wizarani kwa mchakato wa **Samia Kalamu Awards**)* |

## 5. HITIMISHO

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**

Wizara kupitia LATRA imeazimia kuendelea kuandaa Maadhimisho ya Wiki ya Usafiri Endelevu Ardhini, sambamba na siku ya Usafiri Endelevu Duniani inayoadhimishwa Novemba 26 kila Mwaka. Maadhimisho haya ni muhimu kwa Wadau wa Sekta ya Uchukuzi, na hasa wa Usafiri Ardhini, ili wapate Jukwaa la kujifunza, kubadilishana uzoefu, ili kuwaunganisha kuwa wamoja zaidi katika kujadili na kukubaliana masuala yao.

Wadau wa Sekta ya Uchukuzi Nchini wanampongeza sana Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, kwa kuchaguliwa tena kuongoza Serikali ya Awamu ya Sita, Kipindi cha Pili. Tunaomba umfikishie salamu hizi za Pongezi na kumtakia Kheri katika Uongozi wake, na kuwa tunamuombea afya njema, hekima zaidi, uvumilivu, na Mwenyezi Mungu ampe subira njema kwenye kazi zake.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**

Nikuhakikishie tu kwamba Wizara ya Uchukuzi kupitia LATRA, itaendelea kusikiliza na kutatua changamoto za Wasafirishaji na Kampuni za Usafirishaji Nchini, na pia itaendelea kuwashika mkono vijana maarufu kama "Maafisa Usafirishaji" kupitia Vyama vya Ushirika wa Wasafirishaji katika Mfumo wa Kuweka na Kukopeshana (SACCOS) kwa makundi bajaji na bodaboda. Vyama hivi vimeshaanzishwa kwa uratibu wa LATRA katika mikoa ya Kilimanjaro (KIBABOT), Mwanza (UWAMWA), Dar es Salaam (UMAPIDA), na Dodoma (UMAPIDO). Lengo kuwahamasisha vijana hawa kuwa katika makundi ya mfumo wa SACCOS ni kuwatambua, maeneo yao ya utoaji huduma, kuwapa elimu juu ya Sheria na Kanuni za Udhibiti wa vyombo vyao, kuhamisha utii wa sheria bila shuruti, kuvaa kofia ngumu (helmet), na kutopakia abiria au mzigo zaidi ya idadi iliyoruhusiwa kisheria, kuweka utaratibu wa kujisimamia wenyewe (self-regulation), na kuwainua kiuchumi.

Aidha, LATRA itaendelea kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria na Kanuni zilizopo, na itaendelea kushirikiana na Jeshi la Polisi, Kikosi cha Usalama Barabarani katika kutekeleza majukumu yake, hususan kupambana na ajali za barabarani.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**

Nashukuru sana kwa fursa hii adhimu ya kusimama mbele yako na hadhara hii kutoa taarifa yangu kuhusu maadhimisho haya.

Ninaomba kuwasilisha.

**CPA Dkt. Habibu Suluo**

**MKURUGENZI MKUU - LATRA**